



# Biashara haramu ya Usafirishaji wa Wanadamu na Utumwa

Biashara haramu ya usafirishaji wa wanadamu ni uhalifu mkubwa nchini Australia.

Biashara haramu ya usafirishaji wa wanadamu na utumwa ni kinyume cha sheria.

Mtu anayetokeleza uhalifu huu anaweza kufungwa jela, awe ni mwanamume au mwanamke.

Ikiwa wewe au mtu unayemjua yuko hatarini, piga simu kwa polisi, nambari ya simu **000**.

Polisi nchini Australia ni salama na wanaweza kuaminika.

Ikiwa unahitaji mkalimani bila malipo piga simu kwa **131 450**.

Serikali ya Australia (Australian Government) haikubali biashara haramu ya usafirishaji wa wanadamu au utumwa wa kisasa katika hali yoyote ile.

Biashara haramu ya usafirishaji wa wanadamu hufanyika wakati watu wanapolazimishwa kuwa katika hali za kutumiwa vibaya kwa faida ya mtu mwingine. Inaweza kuwafanyikia wanaume, wanawake na watoto. Biashara haramu ya usafirishaji wa wanadamu na utumwa inaweza kujumuisha:

- Utumwa, kufanyishwa kazi kwa lazima katika viwanda kama vile vya ukarimu, ujenzi, misitu, uchimbaji, au kilimo, na hata pia mahusiano ya kimapenzi.
- utumwa wa madeni;
- kutumiwa vibaya kimapenzi;
- ndoa ya lazima; au
- biashara haramu kwa lengo la kuondolewa kiungo.

Biashara haramu ya usafirishaji wa wanadamu na utumwa ni uhalifu uliofichwa.

Biashara haramu ya usafirishaji wa wanadamu na utumwa unaweza kuwa mgumu kugunduliwa. Huenda watu wasitafute msaada kwa sababu wanaogopa adhabu kutoka kwa wanaowanyanyasa au kupoteza hali yao ya uhamiaji.

Ishara ambazo zinaweza kuonyesha mtu anasafirishwa kiharamu zinaweza kujumuisha mahali mtu:

- anashurutishwa, kutishwa au kulazimishwa kufanya kazi;
- amepewa hali duni za kufanya kazi;
- halipwi au anaonekana analipia deni kubwa kwa mwajiri wake au mtu mwingine; au
- pasipoti yake au hati zingine za kibinafsi zimechukuliwa na mtu mwingine, na hawezi kupata hati hizi akizitaka.

## Je, wewe au mtu unayemjua yuko hatarini?

Ikiwa wewe au mtu unayemjua yuko katika hatari ya biashara haramu ya usafirishaji wa wanadamu au utumwa, unaweza kuwasiliana na Polisi wa Serikali ya Australia (AFP) (**Australian Federal Police (AFP)**) nambari ya simu **131 237** (131AFP) au nenda kwenye tovuti ya **AFP** kwenye **www.afp.gov.au** kwa msaada. AFP wanaweza kukuweka salama, kukupa ushauri na kukuelekeza kwa huduma nyingine za usaidizi, kama vile malazi, msaada wa kifedha, ushauri na ushauri wa kisheria na uhamiaji.

Mpango wa Msaada kwa Watu Waliosafirishwa Kiharamu (**Support for Trafficked People Program**) umefadhiliwa na Serikali na kutolewa na Msalaba Mwekundu wa Australia (Australian Red Cross) ili kutoa usaidizi kwa watu ambao ni waathiriwa wa biashara haramu ya usafirishaji wa wanadamu au utumwa.

## Kuna huduma zingine nchini Australia ambazo zinaweza kukusaidia.

**1800RESPECT** ni huduma ya ushauri wa mzozo wa kijinsia, uhasama wa kifamilia na kinyumbani kutoka kwa taifa la Australia (Australia's national sexual assault, family and domestic violence counselling service). Hutoa maelezo na ushauri wa mtandaoni na wa simu bila malipo na wa siri. Washauri watakusikiliza, watajibu maswali na kukuelekeza kwa huduma nyingine za msaada katika eneo lako.

Piga simu kwa **1800 737 732** au nenda kwa **tovuti ya 1800RESPECT** kwenye **www.1800RESPECT.org.au**.

## Je, unahitaji mkalimani?

Piga simu kwa **Huduma ya Ufasiri na Ukalimani (Translating and Interpreting Service (TIS))**, nambari ya simu **131 450**. Mkalimani kutoka TIS anaweza kukusaidia kuwasiliana na huduma zingine, hata hivyo TIS haitoi huduma ya ushauri. Simu zote hazilipishwi na ni za siri.

## Maelezo zaidi kuhusu biashara haramu ya usafirishaji wa wanadamu na utumwa nchini Australia:

Kwa maelezo zaidi kuhusu Support for Trafficked People Program nenda kwenye tovuti ya Idara ya Huduma za Jamii (Department of Social Services) kwenye **www.dss.gov.au** au tovuti ya Msalaba Mwekundu wa Australia (Australian Red Cross) kwenye **www.redcross.org.au**. Unaweza pia kutuma barua pepe kwa Msalaba Mwekundu wa Australia (Australian Red Cross) kwenye **national\_stpp@redcross.org.au**.

Kwa maelezo zaidi kuhusu biashara haramu ya usafirishaji wa wanadamu na utumwa, nenda kwenye tovuti ya Department of Home Affairs kwenye **www.homeaffairs.gov.au** au tovuti ya Australian Federal Police kwenye **www.afp.gov.au** na utafute "human trafficking".